BIBLIA KWA TASWIRA, AGANO LA KALE, KITABU CHA 10
KUTOKA, Sehemu ya Tano

HEMA – TASWIRA YA BWANA YESU-KRISTO, Sehemu ya Pili

(VISUALIZED BIBLE, Vol 10, OT, The Tabernacle, Part Two**)**
Mwandishi: Katherine E. Hershey
Muchapaji: Vernon Henkel
Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

© Bible Visuals International
PO Box 153, Akron, PA 17501-0153
Simu: 717-859-1131
www.biblevisuals.org

SOMO 1 - VIFUNIKO VYA HEMA

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Kutoka 26:1-37; 36:8-36; Walawi 16:5-10, 21, 22; Waebrania 7:23-10:22

Shabaa ya somo: Kuonyesha namna Mungu alivyokusudia wafanye Hema sawasawa kabIsaya
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Hema ilifunua Kristo na Kazi yake mia na mia za miaka mbele ya kuja kwake duniani.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu ya kuwa na uhusiano kabisa na Kristo.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Wasioamini: Kumupokea Bwana Yesu kama Mwokozi toka zambi zao.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Hema Takatifu toka inje (Kutoka 26:1-6, 36-37; 36:8-13.)
2. Ndani ya Hema Takatifu (Kutoka 26:15-29; 36:20-36.)
3. Vifuniko vya Hema Takatifu (Kutoka 26:7-14; 36:14-19; Walawi 16:5-10, 21-22.)
4. Vifuniko - Ukumbusho wa Bwana Yesu.

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Muniangalie, na mwokolewe, miisho yote ya dunia; kwani mimi ni Mungu, na hapana mwengine." Isaya 45:22

Maelezo kwa mwalimu:

Hema inafundisha kwamba Mungu ni mutakatifu (Kuta zinafunga Mungu ndani. Kutoka 25:22). Inatufundisha vilevile ya kwamba watu ni wenye zambi, (Kuta zinawafunga inje. Hesabu 3:10). Na inafundisha njia ya pekee kwa mutu kuweza kukaribia Mungu. (ni kwa njia y damu tu, Waebrania 9:22)

Kama ukichagua kufundisha shairi moja tu kwa masomo haya mane, tunashauri ufundishe Yoane 14:6. Usaidie wanafunzi wako kufahamu kwamba sehemu ya mafundisho yako iliyo hadisi si Neno la Mungu. Lakini mambo ya hakika ao kweli ni Neno la Mungu kabIsaya

Ukitumia mifano kagua masomo ambayo ulifundisha mble. Ni neno kubwa kukagua masomo.

Mukaguo:

Kwanza katika masomo haya tulijifunza juu ya mapazia yaliyozunuka kiwanja. Vile tuliona njia moja ya kuingia. Katika somo la pili tuliona vyombo ndani ya kiwanja.

1. Chamobo gani kilikuwa cha kwanza nyuma ya pazia? (Mazabahu ya shaba)
2. Kwa nini iliitwa mazabahu ya shaba? (Kwa sababu ilifunikwa na shaba)
3. Nini ilikuwa chini ya Shaba? (Mbao ya mushita)

4. Mbao na shaba zilikuwa mifano ya Bwana Yesu namna gani? (Mbao ni kukumbusha kwamba Bwana Yesu, Mungu Mwana, aligeuka kuwa mutu. Shaba inatukumbusha kwamba yeye ni nguvu. Hageuzi nia yake juu ya zambi kamwe - anaichukia saa zote.
5. Kwa nini mwana-kondoo anatukumbusha juu ya Bwana Yesu? (Yeye ni Mwana-Kondoo wa Mungu aliyekufa kwa zambi ya ulimwengu)
6. Hata zabihu za nyama zinatukumbusha ya kufa kwa Bwana Yesu musalabani, nini ni tofauti katikati yao? (Zabihu za nyama zilitolewa tena na tena, zabihu ya Kristo ilitolewa kwa zambi mara moja tu.)
7. Vitu gani vingine vilikuwa ndani ya kiwanja? (Birika na tako lake). Birika na tako lake yalitumia kwa nini? (Makuhani walinawa na miguu yao pale.) Nini ilitumiwa kufanya birika na tako lake? (Vioo vya wanawake)
8. Kwa nini birika linatukumbusha juu ya Bwana Yesu? (Wakati tunapoangalia kioo - maisha kamilifu ya Bwana Yesu - tunaona kwamba sisi ni wenye zambi kabisa).
9. Kunawa kwa birika kuna maana gani kwetu? (Nyuma ya kuzaliwa katika jamaa ya Mungu tunafanya zambi tena. Sharti tukiri zambi zile kwa Mungu ili tusafishwe tena.) (Mwalimu: Ni neno kubwa wanafunzi wafahamu maulizo haya. Uwakague)

Somo: Finehasi alikuwa na njaa. Kunusa chakuna mama yake alipiga kwa hema yao kulimupa njaa kabisa Aliuliza: "Baba atarudi saa gani?"

Mama aljibu na kuchekelea: "Mbio sasa, kisha tutakula."

Finehasi aliuliza: "Mama unafurahi kwa sababu baba ni kuhani?"

"Ee, ndiyo, Finehasi! Ni heshimu kubwa kwake kutumikia Mungu aliye hai na wa kweli. Ninafurahi kwa sababu yeye ni kuhani."

Finehasi alisema: "Ninafurahi vilevile. Anajibu maulizo yangu yote juu ya Hema Takatifu." Akiinamisha kichwa chake, alisema: "Upande wa inje ya Hema haionekane vizuri sana, sivyo mama?"

1. Hema Takatifu toka inje (Kutoka 26:1-6, 36-37; 36:8-13.)

Mama alitikisa kichwa chake: "Hapana. Upande wa inje si muzuri. Lakini baba yako anaweza kutuambia juu ya upande wa ndani, na pale ni pazuri sana."

Onyesha taswira 1: Nyuma, wakati walipokula chakula cha mangaribi, baba yake aliwaambia juu yake. "Pazia kwa mulango wa Hema ni sawasawa na lile kwa mulango wa kiwanja. Linatandikwa juu ya nguzo tano zilizofunikwa na zahabu."

Finehasi aliinamisha kichwa chake: "Ninajua, Baba, nguzo zinafunikwa na zahabu. Ni nzuri sana. Ninaweza kuziona toka mulango."

2. Ndani ya Hema Takatifu (Kutoka 26:15-29; 36:20-36.)

Onyesha taswira 2: Eleazari alisema tena: "Hema inagawiwa kwa sehemu mbili. Pazia nzito sana linagawa vyumba viwili. Kama pazia juu ya dari, pazia hili vilevile linafanywa na makerubi. Kuta za Hema ni mbao zinazofunikwa na zahabu. Zinafungwa pamoja inje na miti, inayolinganishwa na pete za zahabu. Finehasi ukumbuke zahabu inatukumbusha kila mara juu ya Mungu na utukufu wake wa haki."

Hapa ni kweli nyingine kwa sisi kujifunza. Biblia inafundisha kwamba wale wanaoamini Bwana Yesu Kristo "wanafichwa na Mungu katika Kristo." Hii mbao zinazofunikwa na zahabu ni mufano wa waamini wanaofichwa katika haki ya Mungu. Kumbuka zilikuwa mbao moja moja. Lakini zililinganishwa na miti kufanya jengo moja. Hivi Kristo anafanya wote ambao wanamwamini kuwa mumoja - mwili mumoja, jengo moja, kanisa moja. (Ona 1 Wakorinto 12:12-13; Waefeso 1:22-23; 2:19-22; 5:30). Hema ilikuwa pahali Mungu alipokaa. Hivi wote wanaoamini ni kao wa Mungu. (Ona 1 Wakorinto 6:19-20).

Eleazari alieleza kwa mwana wake namna mbao zilivyofungwa pamoja. Alisema: "Mbao zilizofunikwa na zahabu zilitiwa ndani ya matako ya feza."

Siku zile, zaidi ya mali yao ilikuwa feza. Walitumia feza kununua vitu vyao. Wakati Biblia inaposema juu ya bei, inatumia neno "Ukombozi". Kwa mufano "mumekombolewa… si kwa feza lakini kwa damu ya damani… ya Kristo" (1 Petro 1:18-19. Bei ya matako ya Hema ilikuwa $ 170,000 katika mali ya Amerique. Bei

kubwa! Lakini Bwana Yesu Kristo alilipa bei zaidi ya ile kwa sisi. Alitoa maisha yake na kutununua na damu yake ya damani.

Mbao zilisimama katika matako ya feza na waamini wanapumuzika katika Kristo aliyelipa na damu yake kwa zambi za ulimwengu.

3. Vifuniko vya Hema Takatifu (Kutoka 26:7-14; 36:14-19; Walawi 16:5-10, 21-22.)

Sasa tusikilize Finehasi tena wakati anaposemezaa na baba yake. "Mama na mimi tulikuwa tukisemezana juu ya kifuniko cha Hema. Hakionekani vizuri, sivyo."

"Hapana, mwana wangu. Lakini ni nguvu kwa sababu kinafanywa na ngozi za pomboo. Kifuniko hiki cha ngozi ya pomboo kinalinda hema isiharibike na hewa, jua, mvua, mawingu, baridi, na vivi hivi."

Finehasi alikumbuka kwamba viatu vyake vilikuwa vya ngozi ya pomboo. Vilikuwa nguvu vilevile na kulinda miguu yake.

Wewe ni tayari kwa ukumbusho mwengine wa Bwana Yesu? Biblia inasema: "Yeye hana sura wala uzuri hata tumutamani" (Isaaya 53:2). Alionekana sawa mutu tu wakati alipokaa hapa duniani. Watu hawakujua kwa Bwana Yesu kwa sababu ya kuonekana wake. Lakini alikuwa mutu muzuri sana, na mwenye nguvu. Analinda watu wake siku kwa siku.

Finehasi na baba yake walisemezana juu ya vifuniko vingine. Kile chini ya ngozi ya pomboo kilikuwa ngozi ya kondoo dume iliyotiwa rangi nyekundu. Eleazari likumbusha mwana wake: "Wanatumia kondoo kwa zabihu."

Fineahsi aliinamisha kichwa chake. "Ninajua. Na kifuniko cha rangi nyekundu kinatukumbusha juu ya zabihu inayokufa kwa pahali pa mwenye zambi."

Finehasi anasema: "Ninaweza kuona kifuniko cha nyuma kutoka mulango. Sehemu yake inatandikwa juu ya pazia linalokuwa mbele ya hema."

Eleazari alieleza: "Ndiyo, Finehasi, na kile ni kifuniko kinachofanywa na nyole za mbuzi."

Onyesha taswira 3: Baba aliendelea kusema: "Mbuzi wawili wanatumiwa kila mwaka kwa siku ya Upatanisho. Kuhani anaweka mukono wake kwa kichwa cha mumoja wa mbuzi wakati anapokiri zambi za watu. Mbuzi yule anauawa na kutiwa kwa mazabahu. Kisha kuhani anaweka mukono juu ya kichwa cha mbuzi ingine na kukiri zambi za watu tena. Kisha mbuzi yule anapelekwa kwa jangwa kupotea na kusahauliwa kwa milele. Mungu anafunika zambi zetu na damu ya zabihu. Anasahau zambi zile vilevile."

Finehasi alisikiliza maneno haya yote. Kifuniko cha nyole za mbuzi kianchofunika upande wa mbele ya hema kitakumbusha daima kwamba Mungu anafunika zambi na kuzisahau. (Ona mufano wa kwanza).

Eleazari alisema: "Kifuniko cha ine kwa upande a ndani ni kizuri kuliko vyote vingine. Wachache tu wameaona kifuniko kile."

Finehasi alijua kwa nini wachache tu walikiona. Kiliwekwa kuonwa ndani ya Hema tu. Na makuhani tu waliweza kuingia kwa Hema.

Onyesha taswira 4: Kifuniko hiki kizuri sana ni dari ya hema. Ni kama pazia kwa mulango kidogo - lakini ni kizuri kuliko. Nyuzi za rangi za samawi, zambarau, na nyekundu zinasokotwa ndani ya kitani kizuri. Mifano ya makerubi inafanywa ndani yake.

(Finehasi alijua kwamba makerubi walikuwa malaika. Alikumbuka Adamu na Hawa waliondoshwa toka shamba la Edeni wakati walipofanya zambi. Makerubi waliwekwa kwa lago la shamba wasiweze kuingia tena.)

Eleazari alisema: "Kifuniko hiki kinafanywa na mapazia kumi. Yanafungwa ao kuunganishwa na matanzi ya zahabu." Finehasi alifunga macho yake nguvu. Alitaka kuwaza namna ilivyokuwa - samawi, zambarau, nyekundu, makerubi, na matanzi ya zahabu. Aliwaza juu ya vifuniko vingine vilevile.

4. Vifuniko - Ukumbusho wa Bwana Yesu.

Wakati Finehasi anapowaza juu ya vifuniko vine, utapenda kuwaza juu ya Bwana Yesu? Watu wengine wanawaza juu yake kama mutu tu. Watu wale hawamutamani. Yeye kama kifuniko cha pomboo tu kwa wao.

Kwa wengine Bwana Yesu ni yule aliyekufa kama zabihu kwa zambi. Wanajua maneno haya ni kweli. Lakini hawakumupokea kama yule aliyekufa kwa zambi zao wenyewe. Kifuniko cha pili cha ngozi ya dume iliyotiwa rangi nyekundu kinawakumbusha kwamba Yesu alikufa - neno lile tu.

Kisha kuna wale walipokea Bwana Yesu kuwa Mwokozi wao. Wamesafishwa toka zambi na damu yake. Kifuniko cha ngozi ya mbuzi ni ukumbusho kwao kwamba Kristo alitoa maisha yake wakati alipokufa kwa pahali pao.

Kuna wengine walioamini Kristo kuwa Mwokozi wao, na wanaotaka sana kumujua zaidi. Wanasoma Neno la Mungu kila siku. Wanaomba kwake kila siku. Wanakwenda kwa kisomo na Ecole du Dimanche kujifunza maneno mengine juu yake. Wanamutii. Wanamwamini kuwaongoza. Watu namna hii wamekwisha kuona uzuri wake. Wanafahamu kifuniko cha ndni cha Hema.

Kila mutu hapa leo ni mumoja wa makundi haya mane. Wewe ni ndani ya kundi gani?

SOMO 2 - PAHALI PATAKATIFU

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Kutoka 25:23-29; 26:31-35; 30:1-8; 36:35-36; 37:10-28; Yoane 6:35; 8:12; Waebrania 7:25.

Shabaa ya somo: Kuonyesha vyombo katika Pahali Patakatifu ni mufano wa Kristo na matendo yake kwa watu wake.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kama Bwana Yesu-Kristo anakuwa nuru, chakula, na muteteaji wa wanaoamini.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu ya kumujua zaidi huyu Bwana anayerizisha kamili.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kufwata "Nuru ya dunia," kukula "Mukate wa uzima" kwa njia ya kujifunza Neno la Mungu, na kumwamini kabisa Yeye anawaombea.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)

1. Pazia (Kutoka 26:31-35; 36:35-36.)
2. Meza ya mukate wa onyesho (Kutoka 25:23-30; 37:10-16; Yoane 6:35.)
3. Kinara (Kutoka 25:31-39; 37:17-24; Yoane 8:12.)
4. Mazabahu ya kuchoma uvumba (Kutoka 30:1-8; 37:25-28; Waebrania 7:25.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Hekalu la Mungu lina mapatano gani pamoja na sanamu? Kwani ninyi ni hekalu ya Mungu aliye hai." (2 Wakorinto 6:16a)

Maelezo kwa mwalimu:

Mafundisho ya mifano ya Biblia ni neno kubwa na la faida. Paulo wakati alipoandika maneno ya historia alisema, "maneno haya yaliwapata kama mifano, yakaandikwa kwa kutuonya sisi" (1 Wakorinto 10:11). Mifano inatuambia tusikose sawasawa wao walivyokosa. Inatufundisha kweli za roho na mafundisho ya roho. (Ona Waroma 15:4)

Mifano ni zaidi habari ya Kristo na kweli juu yake. (Ona 1 Wakorinto 10:14). Ndani ya Ebrania 9 tunaona sababu ya kutumia Hema kama mufano ni kwa Waebrania 9. Ni neno kubwa kuona kwamba ni ni mufano wa "Hema ya kweli" mbinguni. (Ona Waebrania 8:2; 9:24)

Ukumbushe mifano katika masomo mengine. Sema zaidi juu ya rangi na madini (zahabu, feza, shaba). Inafaa uulize juu ya mbao zinazofunikwa na zahabu na kila kifuniko cha Hema ni mufano wa Kristo. Vizuri wanafunzi wajue maneno ya vifuniko, lakini ni afazali wajue namna yao.

Somo: Finehasi aliketi karibu na mulango wa Hema. Hakuwa peke yake siku hii. Rafiki walikuwa pamoja naye. Walisemezana juu ya maneno mengi - kazi nguvu waliyofanya kwa Misri na namna walivyopigwa na Wamisri. Walisema juu ya usiku wa Pasaka. Walizungumuza juu ya ajabu Mungu alilofanya kwa Bahari Nyekundu. Kwa mwisho walisema juu ya Hema Takatifu.

Kijana mumoja alisema: "Unakupasa kujua maneno mengi juu ya Hema, Finehasi, kwa sababu baba yako ni kuhani. Kuhani anaweza kuingia hata ndani ya Hema. Tafazali utuambie juu yake."

Finehasi alijibu: "Ninaweza kuwaambi ninyi maneno mengine. Nimeuliza baba yangu maneno mengi."

Mwengine alisema: "Ni namna gani ngambo ya pazia lililo mulango? Nimesikia kuna vyumba vilevile."

Finehasi aliinamisha kichwa chake: "Ndiyo, kuna vyumba viwili. Chumba cha kwanza - kile ndani ya pazia - ni Pahali Patakatifu. Chumba kile ni kikubwa kuliko kingine. Nyuma ya Pahali Patakatifu ni pazia lingine."

1. Pazia (Kutoka 26:31-35; 36:35-36.)

Wengine walisema, "Pazia ni namna gani?"

Onyesha taswira 5: Linafanana na pazia kwa lango na mulango, lakini ni nzuri kuliko. Ni sawa na kifuniko juu ya Hema - lakini si mapazia mbalimbali lakini sehemu moja tu.

Finehasi alifikiri rafiki zake hawakujua maneno mengi juu ya pazia. Baba zao hawakuwa ndani ya Hema kwa sababu hawakuwa makuhani. Hivi Finehasi aliaza kueleza juu ya nyuzi za rangi mbalimbali zilizosokotwa ndani ya kitani kizuri na mufano wa makerubi iliyoshonwa ndani yake.

Kijana mumoja alisema: "Ee, ninajua, mama yangu alisaidia kufanya pazia ile. Alisokota na kufuma. Alisaidia kufanya hata makerubi." Wengine walimwangalia na kushangaa. Vijana walijua Mungu alitafuta wanawake na mioyo ya kutaka. Aliwapa akili kufanya mapazia na vifuniko vya Hema. (Ona Kutoka 35:25-29.) Wengine waliokuwa na akili kabisa walifanya mapazia na makeubi. Kijana alisema na sauti polepole: "Kufikiri ya kwamba mama yangu alisaidia kufanya pazia lililotandikwa katika Pahali Patakatifu." Macho yake yalingaa wakati alipowaza juu ya namna ilivyoonekana.

Mutu mwengine alisema: "Ni nana gani kwa upande wa pazia?"

Finehasi alieleza: "Chumba nyuma ya pazia pa Pahali Patakatifu ni Pahali Patakatifu Sana." Alitikisa kichwa chake akisema: "Sijui ni namna gani. Unaona hata baba yangu hawezi kuingia pale." Vijana walishangaa. Finehasi aliendelea kusem:, "Kuhani mukubwa tu anaweza kuingia Pahali Patakatifu Sana na anaweza kuingia mara moja tu kila mwaka. Lakini babu yangu Haruni ni Kuhani mukubwa. Siku moja ataniambia juu ya chumba kile."

Kisha Finehasi alisema kwa sauti ndogo: "Wakati babu Haruni anapokufa baba yangu atakuwa Kuhani mukubwa." Vijana walikaa kimya saa ndefu. Wakati Finehasi aliposema tena, sauti ilikuwa chini kuliko: "Na wakati baba yangu anapokufa, nitakuwa Kuhani mukubwa." Vijana walikuwa kimya kwa saa ndefu kabIsaya Ilikuwa neno la maana sana! Lakini lilikuwa neno nzuri kabIsaya

2. Meza ya mukate wa onyesho (Kutoka 25:23-30; 37:10-16; Yoane 6:35.)

Vijana wangali walikuwa na maulizo. "Utuambie maneno mengine juu ya chumba cha kwanza - Pahali Patakatifu. Baba yako anajua nini ni ndani yake?"

Onyesha taswira 6: Kwa upande wa kaskazini (kwa kuume wakati makuhani wanapoingia) ni Meza ya Mukate wa Onyesho.

Kijana moja aliuliza: "Inafanywa na nini? Inaonekana namna gani?"

"Meza ya Mukate wa Onyesho inafanywa na mbao na inafunikwa na zahabu. Ina ukingo wa zahabu kama taji ya zahabu inayozunguka meza. Inaitwa Meza ya Muakte wa Onyesho kwa sababu kila siku ya sabato mikate kumi na miwili iliwekwa juu yake."

Kijana mwengine alitaka kujua: "Maana ya mikate kumi na miwili ni kwa makabila yetu kumi na miwili?"

Finehasi alisema: "Ndiyo ni maana yao."

"Nini inatokea na mikate ya kwanza wakati wanapokwenda na mikate mipya?"

"Ni chakula kwa makuhani. Pale kwa Pahali Patakatifu wanakula mikate wanayoondosha kwa meza."

Tusimame kidogo kusemezana juu ya mikate na namna inavyokuwa mufano wa Bwana Yesu. Ni wazi. Yesu alisema, "Mimi ni mukate wa uzima, yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa" (Yoane 6:35.) "Kama mutu akikula mukate huu atakaa milele" (Yoane 6:51.)

Tufanye mukate, sharti ngano ipondwe na kusagwa kwanza. Kisha itapigwa pamoja na vichanganyiko vingine. Tena itatobolewa na kanya. Kwa mwisho inaingizwa kwa jiko. Maneno haya yantukumbusha juu ya maumivu ya Bwana wetu Yesu. Unakumbuka namna alivyopigwa? (Mwalimu, unaweza kusema maneno mengine juu ya mateso yake kama ukitaka.)

Yesu ni mukate wa Mungu aliyetoka mbinguni sawasawa alivyosema. (Ona Yoane 6:33) Wakati tunapoendelea kumujua, tukisoma Neno lake, tukiishi kwa yeye, tunakumula kama makuhani walivyokula mikate ya onyesho. (Mukumbuke sisi ni makuhani vilevile).

3. Kinara (Kutoka 25:31-39; 37:17-24; Yoane 8:12.)

Kijana mwengine aliuliza: "Nini nyingine ni katika Pahali Patakatifu?"

Onyesha taswira 7: Finehasi alijibu: "Unajua ya kwamba, hakuna madirisha katika hema, lakini kuna taa katika Pahali Patakatifu. Kwa upande wa kusini (kwa upande wa kushoto wa makuhani wakati wanapoingia) ni

kinara cha zahabu. Ni ya damani. Baba yangu anasema ni kadiri ya talenta ya zahabu." (Kama Finehasi angalisema kwa wakati wetu, angalisema $ 145,600.) Wakati alisema hivi, macho ya vijana yalifunguliwa wazi kabisa!

Finehasi alieleza: "Ni kinara kizuri kabIsaya Kinafanywa na zahabu inayofuliwa na kina maua na matawi mazuri sana yanayochorwa juu yake. Kunamabakuli saba kama maua ya lozi - moja juu ya kila tawi - yanabeba mafuta. Ullimi mudogo wa moto unachoma katika kila bakuli. Nuru inawaka daima. Inachoma atika Pahali Patakatifu muchana na usiku."

Kinara kinakukumbusha juu ya Bwana Yesu Kristo? Zahabu ya kinara inaonyesha kwamba Yeye ni Mungu Mwana. Kinafanywa na zahabu inayofuliwa, inayosema juu ya mateso yake. Yeye ni nuru ya ulimwengu - nuru inayongaa daima. Bwana Yesu alisema: "Yeye ambaye ananifuata hatakwenda kwa giza kabisa, lakini atakuwa na nuru ya uzima." (Yoane 8:12.)

4. Mazabahu ya kuchoma uvumba (Kutoka 30:1-8; 37:25-28; Waebrania 7:25.)

Finehasi alieleza: "Kuna chombo kimoja kingine katika Pahali Patakatifu. Ni mazabahu ya zahabu ao mazahabu ya kuchoma uvumba." Finehasi aliona vijana kuangalia mazabahu ya shaba. Alitikisa kichwa chake, akisema: "Ee hapana! Mazabahu ya kuchoma uvumba si kama mazabahu ya shaba hata kidogo."

Onyesha taswira 8: Aliendelea kusema: "Ni ndogo kabIsaya" (Mwalimu, ilikuwa nusu ya metre carré na metre moja juu. Linganisha kipimo chake na kitu wanafunzi watakachojua.) "Zabihu za nyama hazichomwe juu ya mazabahu ya zabihu - uvumba tu. Baba yangu anasema kuna harufu tamu inauka daima katika Pahali Patakatifu kwa sababu uvumba unachomwa saa zote. Makaa yanyoungua juu ya mazabahu hii yalitoka mazabahu ya shaba.

Mutu aliuliza,: "Mazabahu ya kuchoma inafanywa na zahabu tu?"

Finehasi alieleza: "Hapana, mazabahu inafanywa na mbao na inafunikwa na zahabu. Ina ukingo ambao unaizunguuka kama taji - sawasawa na meza ya mukate wa uonyesho."

Si vigumu kwako kufahamu mufano huu wa Bwana Yesu. Mbao zilizofunikwa na zahabu zinaonyesha kwamba Bwana Yesu ni Mungu na mutu. Lakini taji inatukumbusha kwamba siku moja atatiwa taji awe mufalme wa wafalme.

Mufano mwengine hautakuwa mugumu kwa wewe kufahamu vilevile - kama ukisikiliza kwa uangalifu. Mara nyingi katika Biblia maombi inaoitwa uvumba. Mara moja tunasoma: "Maombi yangu yawekwe kama uvumba mbele yako" (Zaburi 141:2). Hivi uvumba wenye harufu tamu unatukumbusha juu ya maombi ya Bwana Yesu. "Yeye ni hai siku zote apate kuwaombea" (Waebrania 7:25). Sawasawa uvumba uliyoungua siku zote katika Pahali Patakatifu, vivyo hivyo Bwana Yesu anaomba sik zote kwa wale walio wake. Anajua maneno yote magumu yanayoingia katika maisha yako. Anajua kila jaribu. Kwa sababu anakuombea siku zote, huhitaji kushindwa na jaribu lolote. Umekwisha kuahidi kuombea mutu na ulisahau? Bwana Yesu hasahau kukuombea kamwe.

Ilikuwa lazima kwa vitu vitamu vilivyotiwa juu ya mazabahu kupigwa na kuchomwa ili vitoe harufu nzuri. Makaa kutoka mazabahu ya shaba katika kiwanja yalitumiwa kuwasha moto juu ya mazabahu ya zahabu. Mazabahu ya shaba inasema juu ya kufa kwa Bwana, zabihu yake. Hii sharti Bwana Yesu awe mwokozi aliteswa mbele ya kuwa Mwokozi ambaye anatuombea.

Alikufa kama zabihu yako. Umekwisha kumupokea aliyeotoa maisha yake kwa zambi zako? Kama sivyo, utafanya sasa hivi?

Onyesha taswira ndani ya kifuniko cha mbele: Katika somo letu leo tulikuwa na mifano mitatu ya Bwana Yesu. Tuwaze juu yao tena.

(1) Meza ya Mukate wa Onyesho inatusaidia kukumbuka yeye ni Mukate wa Uzima.
(2) Kinara kinatukumbusha kwamba yeye ni Nuru ya Ulimwengu.
(3) Mazabahu ya Uvumba inasema kwamba yeye aliye hai kwa milele anatuombea.

Haya ni kweli nzuri sana kama umekwisha kuamini Bwana Yesu. Kama hukuamini kweli hizi si kitu kwako. Utapenda kumwamini leo? (Mwalimu, uwaonysehe wazi njia ya kuamini.)

SOMO 3 - PAHALI PATAKATIFU SANA

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Kutoka 25:10-22; 37:1-9; 16:32-34; Walawi 16:1-22; Hesabu 17:1-10; Torati 10:2, 5; Waebrania 9:4, 7-15; 10:1-14, 19-22.

Shabaa ya somo: Wanafunzi waweze kujifunza kwamba kuna pahali pa kukutana katikati ya Mungu mutakatifu na mwenye zambi.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Hakuna mutu anaweza kukaribia Mungu bila zabihu za damu kwa ajili ya zambi.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kuwa mwenye zambi na shukrani kwa sababu ya kusamehewa zambi bila malipo kwa njia ya damu ya Yesu.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Wasioamini: Kutegemea Bwana anayeondoa zambi na damu yake. Walioamini: Kuwa na kusudi katika juma huu ya kupatia mumoja wa rafiki zake habari ya wokovu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Sanduku ya Agano (Kutoka 25:10-22; 37:1-9.)
2. Ndani ya sanduku ya Agano (Kutoka 16:32-34; Hesabu 17:1-10; Torati 10:25; Waebrania 9:4.)
3. Siku ya Upatanisho (Walawi 16:1-22.)
4. Bwana Yesu Kristo na Siku ya Upatanisho (Waebrania 9:7-15; 10:1-14, 19-22.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Kwa sababu Kristo hakuingia katika Pahali Patakatifu palipofanywa na mukono, ndio mufano wa kweli, lakini aliingia mbinguni zenyewe, aonekane sasa mbele ya Mungu kwa ajili yetu" (Waebrania 9:24)

Maelezo kwa mwalimu:

Simulia na wanafunzi wako juu ya mifano mikubwa inayokwisha kuonyeshwa katika mafundisho ya Hema. Sheria kubwa ya kufundisha ni: Kagua, kagua, kagua!

Wakati unapokuwa karibu kumaliza somo hili, eleza kwamba hekalu katika Yerusalema liliingia kwa pahali pa hema katika jangwa. Pazia lililopasuka wakati Kristo alipofufuka halikuwa ndani ya hema. Lilikuwa katika hekalu lililokuwa na vyombo sawa, na kuabudu kulikuwa sawa. (Ona Mambo ya Siku 3:1-5:14)

Somo: Finehasi alikuwa akingoja siku hii kwa siku nyingi. Babu Haruni, kuhani mukubwa, alikuwa akikuja kwa hema ya Finehasi. Na babu yake atajibu maulizo yake juu ya Hema Takatifu. Finehasi alijua mazabahu ya shaba na birika zilikuwa kwa kiwanja. Alikumbuka namna vifuniko vilivyofanywa na ngozi mbalimbali. Aliweza kusema nini vilikuwa kwa Pahali Patakatifu. Lakini Finehasi hakjua nini ilikuwa ngambo ya pazia katika Pahali Patakatifu Sana - Babu yake ataweza kumwambia juu yake.

Nyuma ya kufika kwa Haruni, Finehasi alikuwa tayari kumwuliza: "Babu, ni namna gani katika Pahali Patakatifu Sana katika Hema Takatifu?"

Babu alichekea. Wakati aliposema, sauti yake ilikuwa polepole na ya kutoa heshima. "Hakuna taa, wala kinara, wala dirisha katika Pahali Patakatifu Sana. Lakini giza si pale. Nuru namna nyingine inajaza pahali pale. Nuru inayotoka Mungu. Ni alama kwamba yeye ni pamoja nasi."

Finehasi alipumzika, lakini hakusema kitu.

1. Sanduku ya Agano (Kutoka 25:10-22; 37:1-9.)

Onyesha taswira 9: Babu Haruni alendela kusema: "Katika Pahali Patakatifu Sana kuna chombo kimoja lakini ni kwa sehemu mbili. Sehemu yake ya chini inaitwa Sanduku ya Agano. (Maana ya agano ni kupatana). Ni sanduku inayofanywa na mbao, na kufunikwa na zahabu. (Mwalimu: Urefu wake ulikuwa 1.1 metres na

upana 0.7 metre na 0.7 metre juu. Linganisha na kitu cha kipimo kile ambacho wanafunzi wako wanaweza kuona.)

Sehemu ya juu iliyofanywa na zahabu safi, iliitwa Kiti cha Rehema. Ni kama kifuniko kwa sanduku. Ni kizuri sana. Kwa miisho miwili ya Kiti cha Rehema ni makerubi zilizofanywa ya zahabu safi. Makerubi wawili yanatazamana. Mabawa yao yananyoshana. Finehasi, hii ni sehemu bora kuliko sehemu zote nyingine za Hema."

"Babu, kwa nini?"

Haruni alijibu: "Mungu alimwambia Musa namna kufanya Kiti cha Rehema. Saa ile aliahidi: 'Nitakutana nawe juu ya Kiti cha Rehema, toka katikati ya makerubi mawili!' Ni hapa utukufu wa Mungu unapokaa. Finehasi, ni kwa sababu hii, sehemu hii ya Hema ni bora kuliko zote nyingine."

2. Ndani ya sanduku ya Agano (Kutoka 16:32-34; Hesabu 17:1-10; Torati 10:25; Waebrania 9:4.)

Onyesha taswira 10: Babu Haruni aliendelea kusema: "Ndani ya Sanduku ya Agano ni mbao za amri kumi. Kuna vilevile pishi ya zahabu iliyo na mana." (Kwa nini Mungu aliamuru watu wake kuchunga mana katika sandukuu ya Agano? Ona Kutoka 16:32)

Wakai Haruni alipoeleza maneno haya yote, hakujua ya kwamba nyuma, kitu kingine kitawekwa ndani ya Sanduku ya Agano. Lakini unaweza kujua, kama ukisikiliza vizuri. Nyuma kidogo, Waisraeli wengine hawakupendezwa kwa sababu Haruni na jamaa yake tu walikuwa makuhani. Walisema na majivuno: "Sisi ni watakatifu kama Haruni."

Hivi Mungu alisema na Musa: "Sema nao kwamba mutu toka kila kabila alete fimbo. Sema na kila mutu kuandika jina lake juu ya fimbo yake. Weka fimbo katika Pahali Patakatifu mbele ya pazia. Kesho asubui fimbo moja itakuwa na uzima ndani yake. Mwenye fimbo ile, na kabila lake, ndio wale waliochaguliwa nami kunitumikia."

Asubui Musa alikamata fimbo toka Pahali Patakatifu na kuzipeleka kwa watu. Mara moja watu waliona kwamba fimbo ya Haruni haikuwa fimbo bila uzima tena. Ilichipuka na kuwa na maua na malozi! Mungu alitaka watu wake kukumbuka daima kwamba wale tu ambao aliwachagua watamutumikia. Hivi aliamuru kwamba fimbo yake iwekwe ndani ya sanduku ya Agano pamoja na amri kumi na pishi ya mana.

Munakuwa tayari kwa kumbusho lingine la Bwana Yesu?

(1) Katika Sanduku ya Agano ya zahabu na mbao zinatukumbusha Yesu Kristo ni Mungu na mutu.
(2) Yeye pekee alitii kwa kamili sheria takatifu ya Mungu, amri kumi.
(3) Yeye pekee ni Mukate - Mana – iliyotoka mbinguni.
(4) Yeye ni Ufufuko na uzima, kama ilivyonyeshwa kwa njia ya fimbo iliyopata uzima.

3. Siku ya Upatanisho (Walawi 16:1-22.)

Sasa turudi kwa Finehasi. Alianza kusema, "Babu, ninajua unaingia Pahali Patakatifu Sana mara moja tu kila mwaka, siku ya Upatanisho yetu. Tafazali, utaniambia maneno mengine juu yake?"

Haruni alieleza: "Siku ya Upatanisho ni siku ya heshima sana kuliko siku nyingine za mwaka muzima. Ni siku ya huzuni kwa sababu ya zambi. Ni siku mimi, kuhani mukubwa, ninapokutana na Mungu kwa ajili ya watu wote wa Israeli. Siku hii sivae mavazi yangu mazuri sana ya kuhani mukubwa. Ninavaa nguo ya kitani."

(Finehasi alipenda mavazi mazuri ya babu yake. Mara nyingine aliuliza juu yao. Lakini sasa hivi alitaka kusikia juu ya Siku ya Upatanisho).

Kuhani mukubwa alisema na mujukuu wake: "Kwanza, tunachinja kondoo dume kwa mazabahu ya shaba. Ninakamata damu yake katika kibakuli na kuipeleka ndani ya Pahali Patakatifu. Pale, kutoka mazabahu ya zahabu, ninajaza chetezo na makaa ya kuwaka kwa moto uvumba."

Onyesha taswira 11: Aliendelea kusema: "Wakati ninapoingia Pahali Patakatifu, moshi kutoka uvumba wa kuwaka unafunika Kiti cha Rehema. (Ona Walawi 16:12-13.) Ninachovya vidole vyangu ndani ya damu katika bakuli na kuinyunyiza juu ya Kiti cha Rehema mara moja. Ninachovya vidole vyangu katika damu tena. Mara hii ninainyunyiza kwa udongo mbele ya Kiti cha Rehema. Mara moja… mbili… tatu, ine, tano, sita, mara saba yote ninanyunyiza damu juu ya udongo. Watu wanangojea inje ya Hema. Wakati ninaporudi, wanajua

kwamba kwa sababu nilitii Mungu, alikubali toleo langu. Kama sikupeleka zabihu ambayo Mungu aliitaka, angeniua. Zabihu hii ya kwanza ni kwa mimi na wote wa nyumbani mwangu. Nyuma, ninatoa zabihu kwa watu.

Babu Haruni anaeleza: “Mara hii mbuzi anauawa kwa zambi za watu. Damu yake inakamatwa ndani ya kibakuli vilevile. Ninapeleka damu ile katika pazia ya Pahali Patakatifu Sana. Ninanyunyiza damu mara moja juu ya Kiti cha Rehema na mara saba kwa udongo.”

4. Bwana Yesu Kristo na Siku ya Upatanisho (Waebrania 9:7-15; 10:1-14, 19-22.)

Wakati Finehasi anapofikiri juu ya Siku ya Upatanisho sisi tunataka kufikiri juu ya Bwana Yesu.

Onyesha taswira 12: Kunyunyiza damu mara moja juu ya Kiti cha Rehema kunatukumbusha kwamba Yesu Kristo alikufa mara moja kwa zambi. Katika Biblia, hesabu ya saba mara nyingi inatumiwa kuonyesha kitu ni kikamilifu ao kinatimizwa. Kunyunyiza damu mara saba kunasema Mungu alitimiza maneno ya zambi kabIsaya

Damu ya Kiti cha Rehema ilitosha Mungu juu ya zambi za watu. Kwanza, ilimutuliza kwa sababu watu wamekwisha kumutii Mungu na kufanya maneno ambayo aliwaomba kufanya. Ya pili, Mungu alitulizwa kwa sababu damu juu ya Kiti cha Rehema ilionyesha Bwana Yesu atakayofanya miza za miaka nyuma.

Babu Haruni amekuwa na kitu kimoja kingine kusema: “Wakati ninaporudi mara ya pili kutoka Pahali Patakatifu, watu wanajua Mungu amekubali zabihu kwa zambi zao. Kisha ninaweka mikono yangu juu ya kichwa cha mbuzi aliye hai na kukiri zambi za watu. Mbuzi huyu anatumwa na kupotezwa katika jangwa kwa milele. Zambi zetu zimekwisha kufunikwa na kusahauliwa. Tunafurahi kwa siku hi kubwa, Siku ya Upatanisho!”

Tunataka kujifunza tena maneno mengine juu ya Bwana yetu. Unajua ya kuwa yeye ni Kuhani wetu Mukubwa? Unajua kwamba sisi tuna Siku ya Upatanisho? Biblia inatuambia juu ya maneno haya katika Kitabu cha Waebrania.

Kwa siku ya Upatanisho kuhani mukubwa aliingia mbele ya Mungu katika Pahali Patakatifu sana. Alipeleka pamoja naye damu ya nyama kwa zambi za watu. Hivi, Bwana Yesu (Kuhani mukubwa wetu) ameingia mbele ya Mungu - katika mbingu yenyewe. Lakini damu ambayo aliitoa haikuwa ya nyama. Ilikuwa damu yake mwenyewe ya damani. Alitoa kwa zambi zako na zangu. Lilikuwa toleo moja kwa watu wote kwa milele.

Sasa hatuhitaji siku ya upatanisho kila mwaka. Siku yetu ya upatanisho ilitokea mara moja. Haitafanywa tena. Wakati Bwana Yesu aliposulubiwa, alilipa zambi zetu na uzima wake, damu yake. Ile ilikuwa siku yetu ya upatanisho.

Wakati Kristo alipokufa, kitu chenye kushangaza kilitokea. Pazia katikati ya Pahali Patakatifu na Pahali Patakatifu Sana kwa hekalu katika Yerusalema ilipasuka kutoka juu kufika chini. (Haikuwa kutoka chini kufika juu). Ilikuwa sawa mikono isiyoonekana ilifanya neno hili. Na ni kweli ni Mungu aliyepasua pazia. Kwa sababu Bwana Yesu alitoa damu yake, njia kufikia Mungu ilikuwa wazi kwa milele kwa kila mutu ambaye atamupokea.

Wakati Yesu (Mwana-Kondoo wa Mungu) alipokufa, kazi ya haruni, na kazi ya Eleazari, na nyuma, kazi ya Finehesi, na kazi ya makuhani wengi wengine ilikwisha. Nyuma ya kufa kwa Bwana Yesu Kristo, Mungu hatapokea kamwe zabihu ya nyama. Atapokea zabihu ya Mwana wake tu. Umekwisha kupokea zabihu ya mwana wake kwa zambi zako? Hakuna nyingine itafaa. (Mwalimu: Omba watoto kuamini Bwana Yesu kuwa Mwokozi wao. Eleza njia wazi).

Kama wewe ni katika jamaa ya Mungu, waza juu ya mutu ambaye utapenda kumwonyesha njia kuamini Bwana Yesu. Tuombe pamoja ili Mungu akupe wewe nafasi kumwambia juu ya Mwokozi.

SOMO 4 - KUHANI MUKUBWA

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Kutoka 28:1-8; 43; 39:1-31; Walawi 8:6-9; Waebrania 2:9; 5:1-10; 6:13-20; 7:23-28; 8:1-6; :1-10:22.

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba makuhani wa Agano la Kale hawahitajiki tena kwa sababu Kristo ni Kuhani Mukubwa.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Njia ya pekee ya kukaribia Mungu ni kupitia Yesu Kristo.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu ya kupatia habari ya wokovu kwa wao wanaotafuta Mungu kwa ingine njia.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kupanga namna wanaweza kutumia mifano ya Hema kuleta wengine kwa Mwokozi.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Mavazi ya Kuhani Mukubwa (Kutoka 28:1-14, 31-35, 39-43; 39:1-7, 22-29; Walawi 8:6-7.)
2. Kifuniko cha kifua na Kilemba (Kutoka 28:15-30, 36-38; 39:8-21, 30-31; Walawi 8:8-9.)
3. Bwana Yesu, Kuhani Mukubwa wetu (Wafilipi 2:5-9; Waebrania 2:9; 5:1-10; 6:13-20; 7:23-28; 8:1-6.)
4. Hema nzima: Ukumbusho wa Bwana Yesu (Waebrania 9:1 hadi 10:22.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mutu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi" Yoane 14:6

Maelezo kwa mwalimu:

Katika ukumbusho wako zungumuza juu ya maana ya vitu vya Sanduku ya Agano. Sema juu ya matendo ya kuhani mukubwa kwa Siku ya Upatanisho. Jua ya kuwa wanafunzi wako wanafahamu siku yetu ya upatanisho na nani ni Kuhani Mukubwa wetu. Kumbusha pazia lililopasuka. Kwa sababu hili litakuwa somo la mwisho juu ya Hema, kamata saa kuona kama walifahamu habari zake na kama mafundisho ya hema ilifanya kazi rohoni mwao.

Somo: Finehasi alifurahi kuona makuhani wakifanya kazi yao katika Hema siku kwa siku. Kila mutu alijua kazi yake, na wakati gani ilimfaa kuifanya. Wote walivikwa na kitani nzuri nyeupe kutoka kichwa kufika miguu.

Biblia inasema kitani nyeupe kinatukumbusha haki. (Ona Ufunuo 19:8). Sisi vilevile tunavikwa na haki ya Mungu. Sisi sote ni makuhani. (Ona Ufunuo 1:5-6; 5:9-10). Umesahau neno hili?

1. Mavazi ya Kuhani Mukubwa (Kutoka 28:1-14, 31-35, 39-43; 39:1-7, 22-29; Walawi 8:6-7.)

Onyesha taswira 13: Kwanza babu alivaa sawasawa na makuhani wote walivyovaa: nguo ya kitani nzuri nyeupe. Lakini akitii amri ya Mungu, Musa alitia nguo ya samawi juu ya ile nyeupe ya Haruni. Ngunga za zahabu zilikuwa kwa upindo wa nguo. Katikati ya ngunga kulikuwa mikomamanga. Juu ya joho ya samawi aliweka vazi fupi bila mikono. Liliitwa efodi. Kitani nzuri katika efodi ilifungwa na rangi za samawi, zamabarau na nyekundu, na nyuzi ya zahabu. Ilifungwa juu ya mabega na vitu vya shohamu. Juu ya kila kitu majina sita ya makabila ya Israeli yaliyochorwa. Hivi Kuhani Mukubwa alivaa majina ya makabila kumi na mawili juu ya mabega yake mawili.

2. Kifuniko cha kifua na Kilemba (Kutoka 28:15-30, 36-38; 39:8-21, 30-31; Walawi 8:8-9.)

Onyesha taswira 14: Efodi ilikuwa na mushipa uliyofanywa na nguo nzuri sawasawa. Halafu Musa alifunga kifuniko cha kifua juu ya kifua cha Haruni. Kifuniko cha kifua kilifungwa kwa pahali pake na mikufu

ya zabahu na kamba ya rangi ya samawi. Katika kifuniko cha kifua vilikuwa vitu vya damani kumi na viwili, akiki nyekundu, yakuti ya rangi ya manjano, zumaridi, yakuti, yapsi… na vitu vingine. Vyote vilifungwa kwa zahabu kwa vijazo vyao. Kila kitu cha kumi na viwili kilichorwa na jina moja la makabila kumi na mawili ya Israeli. Kuhani Mukubwa alikuwa na majina ya makabila ya Israeli kwa mabega yake na vile aliyachukua karibu na moyo wake.

Kwa mwisho, Musa alitia kilemba juu ya kichwa cha Haruni. Kilemba kilikuwa na bamba ya zahabu mbele. Finehasi aliweza kuona maandiko juu ya bamba. Akiangalia karibu, aliona, "Takatifu kwa Bwana". Musa alieleza: "Mungu alisema mavazi haya yatakuwa kwa utukufu na kwa uzuri."

Lakini Finehasi babu yake kumwambia maneno mengine juu ya mavazi mazuri sana haya ya kuhani mukubwa. Aliuliza: "Ngunga na matunda yanayozunguka upindo wa joho yana maana?"

"Ndiyo, yana maana. Ngunga zinalia wakati wanapotembea. Wakati watu wanaposikia ngunga, wanakumbushwa Bwana Mungu. Wanajua kwamba ninafanya kazi yake. Ngunga zinasema nao juu yake. Lakini kama ngunga zinaacha kulia, watu watajua nilipigwa hata kufa kwa sababu nilikosa kufikia Bwana kwa njia aliyoagiza!"

Babu Haruni aliendelea kusema: "Makomamanga yanatukumbusha ya kuwa nilichaguliwa katumikia Bwana. Matokeo ya utumishi wangu ni kama matunda kwake."

Sisi hatuvai ngunga kusudi watu wawaze juu ya Bwana. Tunakumbusha juu yake na maneno ambayo tunayosema na namna tunavyoishi. Ngunga zinasema juu ya ushuhuda wetu kwake.

Mungu anataka tuzae matunda. Hatuvai makomamanga. Lakini kama tukikaa karibu na Bwana Yesu na kumushuhudia kwa wengine, tunamuzalia matunda.

Finehasi alitaka kujua: "Majina ya makabila ni juu ya vito kwa mabega, na juu ya vito ya kifuniko cha kifua. Kwa nini?"

Babu Haruni alipumua. Aleleza; "Ni kazi yangu kusimamia watoto wa Israeli. Kama kuhani mukubwa wao, ninasimama katikati yao na Mungu. Bega ni pahali pa nguvu. Maana ya majina juu ya mabega ni kwamba ninataka kuwabeba katika pahali panapokuwa pagumu ndiyo mambo magumu. Ninasemezana na Mungu juu yao kwa maombi. Sisahau kamwe ya kuwa wao ni kazi yangu. Majina juu ya vito kwa kifuniko cha kifua yananikumbusha kwamba ninawachunga karibu na moyo wangu. Moyo ni pahali pa mapendo." Babu Haruni alipumua tena. Kisha alicheka. Alisema: "Ninapenda watu wangu sana."

3. Bwana Yesu, Kuhani Mukubwa wetu
(Wafilipi 2:5-9; Waebrania 2:9; 5:1-10; 6:13-20; 7:23-28; 8:1-6.)

<u>Onyesha taswira 15</u>: Hapa ni mufano muzuri wa Bwana Yesu. Yeye ni mwenye nguvu, amevalishwa taji ya utukufu na heshima. (Ona Waebrania 2:9). Kama ukimupokea kuwa Mwokozi wako, yeye - Bwana wa utukufu - anakuchukua kwa wakati wa taabu. Anakubeba juu ya bega lake - pahali pa nguvu. Yeye anakulinda karibu na moyo wake vilevile kwa sababu anakupenda sana. Kuhani Mukubwa muzuri sana!

Hakuhitaji Finehasi kuuliza juu ya nguo nzuri katika efodi. Amekwisha kujifunza juu ya maana ya rangi kutoka nguo ya Hema. Alifahamu kwa nini Mungu alisema mavazi haya ni kwa utukufu na uzuri. Kuhani mukubwa aliyavaa kila siku ila moja - Siku ya Upatanisho. Kisha wakati alipopeleka damu mbele ya Bwana Mungu kwa zambi za watu, alivaa kitani nyeupe.

Neno hili linatukumbusha juu ya Bwana Yesu vilevile. Wakati alipoishi mbinguni mbele ya kufika duniani, alivikwa na enzi na utukufu. Yeye, Mwana wa Mungu, alikuwa juu ya kila malaika mbinguni. Lakini wakati alipokuja kuchukua zambi zetu aliacha utukufu wake, kama kuhani mukubwa alivyoacha mavazi yake mazuri Siku ya Upatanisho. Nyuma ya kufa kwa zambi zetu, alifufuka toka kaburi. Sasa yeye ni mbinguni. Na anapata tena utkufu ambao alikuwa nao mbele ya kujinyenyekeza mwenyewe na kuja duniani. (Ona Wafilipi 2:5-9)

Finehasi aliwaza tena juu ya wakati Musa alipovalisha tata Haruni na mavazi ya KuhaniMUkubwa. Ilikuwa siku kubwa sana! Ilikuwa siku wakati Hema iliposimamishwa mara ya kwanza. Elfu na elfu za wanaume na wanawake, vijana na wasichana walikuwa pale. Nguo zilifungwa pamoja, nguzo zilisimamishwa, na mazabahu iliwekwa kwa pahali pake. Kisha, wakati kila kitu kilipotimizwa, wingu la utukufu lilijaza Hema. Hakuna mutu aliyewe kuingia Hema, wala Musa wala Kuhani Mukubwa, wakati wingu lilipojaza Hema. Kwani Mungu mwenyewe alikuwa, akijaza pahali pazima. Kwa mwisho, wingu lile lilipanda na kukaa juu ya Pahali Patakatifu

sana. Ilibaki pale kama alama kwamba Mungu alikuwa pamoja na watu wake. Finehasi alijua hatasahau siku ile kamwe.

Umejifunza mambo mengi juu ya Hema - Hema hii nzuri sana inayoweza kuhamishwa huko na huko. Tunatumaini wewe kama Finehasi hutayasahau. Hukuona Hema, wala kushikiana na ibada hii kama Finehasi alifanya. Hivi itakuwa kugumu kwako kukumbuka. Lakini omba Mungu kukukumbusha masomo haya na kweli ambazo ulijifunza.

4. Hema nzima: Ukumbusho wa Bwana Yesu (Waebrania 9:1 hadi 10:22.)

Onyesha taswira 16 na 17: (Mwalimu: Shika kitabu kwa upande na taswira 16 juu. Wakati unapotaja kila chombo, onyesha mufano wake).

Tulijifunza kwamba Bwana Yesu peke yake ni mulango. Mazabahu ya shaba inatukumbusha kwamba yeye ni zabihu yetu ya zambi. Damu yake inatosha kwa zambi zilizopita, zambi za sasa, na hata zambi za kuja! Tunakuja mara moja kwa usamehe wa hukumu ya zambi. Saa ile tunakuwa watoto wake. Birika inatukumbusha kwamba sharti wale walioamini Krsito wafike kwake kila siku kusafishwa. (Ona Yoane 13:6-30; Waefeso 5:25-27.)

Mazabahu ya uvumba ni ukumbusho kwamba Bwana Yesu antuombea. Tunakumbuka kama kuhani mukubwa wetu wakati tunapofikiri juu ya Sanduku ya Agano na Kiti cha Rehema Aliingia mbele ya Mungu - si na damu ya nyama, lakini na damu yake mwenyewe ya damani ambayo alitoa mara moja. Kwa sababu ya kufa kwake na ufufuko wake, wote ambao wanamwamini wana uhuru toka hukumu ya zambi kwa milele.

(Mwalimu: Kwa kumaliza, wakati unaposema Yoane 14:6, onyesha na kidole chako toka mulango ulio chini kwa Kiti cha Rehema kilicho juu, na kutoka kinara kufika meza ya mukate wa onyesho, kuonyesha mufano wa musalaba.)

Bwana Yesu ni njia moja na ya pekee ufika kwa Mungu. Alisema, “Mimi ni njia (Onyesha mulango na mazabahu ya shaba) na kweli na uzima. (Onyesha birika na mazabahu ya uvumba). Mutu hakuji kwa baba (Onyesha Sanduku ya Agano na Kiti cha Rehema), ila kwa mimi.” (Onyesha kinara na meza ya mukate wa onyesho). Hakuna mutu anayeweza kukaribia ungu ila kwa damu ya Mwana wake, Bwana Yesu Kristo. Unaweka imani yako yote ndani yake? Kama sivyo, utafanya hivi sasa?

Kama wewe ni mutoto wake, umekwisha kusema na wengine juu ya kweli za hema? Munaweza kuchapa musalaba kubwa ndani ya buku zenu na vyombo vya Hema. (Mwalimu: tia wanafunzi moyo wa kuchapa vyombo kufwatana na kartasi 16 na 17 ya kitabu hiki.) Kiisha kuchapa munaweza kutumia buku zenu kusemezana na jamaa na rafiki juu ya njia inayofika kwa Mungu: kwa njia ya Kristo, Mwana wa Mungu aliyetoa damu yake kwa ajili ya zambi.